

Unda nywila thabiti

Unahitaji jina la mtumiaji na nywila kuingia kwenye tovuti nyingi. Tumia nywila thabiti kila mara.

Nywila thabiti ni kama gani?

Nywila thabiti:

- ni ngumu kwa watu wengine kukisia
- ina herufi zaidi ya 8
- inatumia herufi, nambari na alama (!@#\$%*)
- ni tofauti na nywila zako nyinginezo.

Usitumie nywila ambazo ni rahisi kukisia. **Usitumie:**

- maneno yanayojulikana na wengi
- nambari zinazofuatana kama 123
- taarifa ya binafsi

Ninawezaje kulinda nywila zangu?

- Tumia nywila tofauti kila mara (mtu hataweza kuingia kenyea akaunti zako zote kwa kutumia nywila moja).
- Usiambie mtu yeyote nywila zako.
- Usiweke nywila zako pahali ambapo watu wengine wanaweza kuziona.
- Toka na ufunge kivinjari chako kama unatumia tarakilishi na wengine au unatumia tarakilishi ya umma.

Naweza je kuunda nywila thabiti?

Kitoka nywila kinaweza kukusaidia kuunda nywila thabiti. Fuata hatua 5 kuunda nywila zako thabiti

- 1. Fikiria kuhusu mshororo wa wimbo unaoipenda au nukuu unaoupenda (Kitabu ni zawadi unayoweza kufungua tena na tena)**
- 2. Tumia herufi ya kwanza ya kila neno (abiagycoaaa)**
- 3. Fanya herufi nyingine ziwe kubwa (AbiagycoaaA)**
- 4. Unaweza kubadili herufi nyingine ziwe alama. Unaweza kubadili herufi nyingine ziwe alama ambazo zinafanana nazo. Kwa mfano, tumia \$ badala ya 's' au @ badala ya 'a'. (Abi@gycoa@A)**
- 5. Ongeza nambari (Abi@gycoa@A5)**

Ninaweza kukumbuka vipi nywila zangu?

Unaweza kutumia kisimamizi nywila kukumbuka na kulinda nywila zako. Lastpass ni mfano wa kisimamizi nywila.

Usikubali vivinjari vya tovuti kuhifadhi nywila zako. Watu wengine wanaweza kufungua akaunti yako kama wanaweza kufikia simu au tarakilishi yako.

Tazama video hii ili kupata maelezo zaidi:

Kiingereza- <https://www.digitalllearn.org/courses/accounts-passwords-new>

Kihispania- <https://www.digitalllearn.org/courses/cuentas-y-contrasenas-nuevo>